

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu: 026 2324343/2324384
Nukushi:0262320046/2320121
Barua pepe : ras@dodoma.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 914
Dodoma

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Uongozi wa Serikali za Mikoa ya Dodoma na Singida Wanaosimamia na Kuratibu Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Kanda ya Kati maarufu kama Maonesho ya Nanenane wameongeza siku mbili (2) zaidi za kuendelea kufanyika kwa Maonesho hayo hadi kufikia Agosti 10, 2017 kwenye Viwanja vya Nzuguni Nje Kidogo ya Mji wa Dodoma badala ya Agosti 8, 2017 iliyokuwa imepangwa awali.

Maamuzi hayo yamekuja kufuatia maombi ya baadhi ya Wajasiriamali, Mashirika, Makampuni na Taasisi zinazoshiriki kwenye Maonesho hayo, pamoja na Wananchi wanaokuja kutembelea Maonesho kulalamika kuwa siku za Maonesho ni Chache na kutoa ombi la kuongezwa kwa siku za kufanyika kwa Maonesho.

Akitangaza Maamuzi hayo kwa niaba ya Wenyeviti wa Kamati Kuu ya Nane Nane Kanda ya Kati ambao ni Wakuu wa Mikoa ya Dodoma na Singida, Mkuu wa Wilaya ya Chemba Mkoani Dodoma ambaye anasimamia kamati inayoratibu Maonesho hayo amesema kuwa shughuli na itifaki zote za kugawa zawadi kwa washindi wa Maonesho ya mwaka huu zitafanyika siku ya Agosti 8, 2017 kwenye Viwanja vya Nzuguni kama ilivyokuwa imepangwa hapo awali na Mgeni Rasmi atakuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa George Simbachawene, lakini baada ya shughuli hiyo, Maonesho yataendelea kama kawaida kwa muda huo wa siku mbili (2) hadi Agosti 10, 2017.

Ameahidi kamati ya Nane Nane Kanda ya Kati kuendelea kuratibu na kusimamia masuala yote muhimu kwa ajili ya Maonesho hayo kuendelea kufanyika na amewakaribisha Wakulima, Wafugaji na Wananchi wa kawaida kutoka Mikoa ya Dodoma na Singida kuendelea kuja kwa wingi kutembelea Maonesho kwenye Viwanja vya Nane Nane Kanda ya Kati hadi Agosti 10, 2017 kujionea Maonesho Mazuri ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi bila kukosa kupita kwenye banda la Maliasili na Utalii linalovutia kwa kuwa na Wanyama hai wa porini wengi kuliko Maonesho mengine yaliyopita lakini Wananchi pia watembelee banda la Afya ambalo linajumuisha Hospitali ya Benjamini Mkapa kujipatia huduma za bure za Upimaji na Tiba kwenye Uwanja wa Nane Nane Nzuguni.

Jeremia Myakyoma

AFISA MAHUSIANO - OFISI YA MKUU WA MKOA DODOMA

Agosti 7, 2017